BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Pili – Tarehe 12 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

29. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani):
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kuchochea maendeleo ya wananchi majimboni, Serikali inatoa fedha za Mfuko wa Jimbo (CDF) kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waliochaguliwa majimboni Unguja na Pemba. Hili limepelekea kuongezeka kwa mahitaji mengi ya wananchi kwenye Afisi za Wawakilishi majimboni hali inayosababisha migongano baina ya viongozi na wananchi wao.

(a) Je, ni vigezo gani vinavyotumiwa na Serikali katika ugawaji wa fedha hizo kwa majimbo ya Zanzibar.

(b) Ni lini Serikali imeufanyia tathmini Mfuko huo tokea kuanzishwa kwake ili kuona matumizi sahihi ya Mfuko huo majimboni.

(c) Ni lini Serikali italeta sheria mpya ya kuuboresha na kuuongezea nguvu Mfuko huo, ili ulingane na hadhi pamoja na mazingira ya mahitaji ya sasa majimboni.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

160. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuzingatia jitihada za Serikali katika kukuza maendeleo endelevu, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha thamani halisi ya fedha katika matumizi ya rasilimali za umma.

(a) Kwa kiasi gani Serikali imejumuisha dhana ya manunuzi rafiki kwa mazingira (Green Procurement) katika mifumo na taratibu za manunuzi ya umma.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa taasisi za umma zinazingatia ununuzi rafiki kwa mazingira wakati wa kufanya manunuzi.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

102. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Katika miaka ya thamanini na tisiini, Zanzibar ilifanya vizuri katika mchezo wa mpira wa miguu kupitia timu za *Small* Simba, Malindi na Mlandege. Mafanikio hayo yalipatikana kwa kutumia makocha na wachezaji wazawa, wakiwemo Abdul Wakati Juma, Karume Mussa, Nassor Ali Kibichwa na Due Said. Hatimae, waliziangusha timu kubwa za Afrika Mashariki zikiwemo Gor-Mahiya, Express ya Uganda na Abaluya ya Kenya.

(a) Je, Soka la Zanzibar limekumbwa na changamoto zipi zilizopelekea Wazanzibari kukakosa furaha ya soka lao na kukimbilia kushabikia timu za nje.

(b) Je, lini Serikali itaanzisha *Football Academy* angalau moja katika kila Wilaya, ili kuwatayarisha vijana katika mchezo wa mpira wa miguu.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

178. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika mwaka huu wa masomo, jimbo la Uzini limepokea wanafunzi wengi sana walioteuliwa kuendelea na masomo yao ya sekondari. Hali hii imepelekea wanafunzi waliopokelewa katika Skuli ya Sekondari Bambi kutumia Ofisi ya Walimu, ukumbi wa mitihani na maktaba kuwa ni sehemu ya kusomea.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga skuli ya ghorofa katika shehia ya Bambi ili kuondosha tatizo liliopo sasa.

185. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tumeshuhudia wanafunzi wengi wanaokaribia kufanya mitihani ya kitaifa kuwekwa kambi katika skuli mbalimbali za Serikali hapa Zanzibar na wakati mwengine bila ya hata kuzingatia jinsia zao.

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuanzisha kambi hizi zinazowekwa katika skuli za Serikali.

(b) Ni vigezo vipi vinavyotumika katika kuanzishwa kwa kambi hizo.

(c) Je, Serikali imefanya tathmini juu ya uanzishwaji wa kambi hizo kiholela na imejiridhisha vipi kuchochea kukithiri kwa vitendo vya udhalilishaji na kimaadili.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

6. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Je, Serikali inatumia juhudi gani kuhakikisha kuwa Polisi na watoa huduma wengine wanapatiwa mafunzo ya kitaalamu ya kushughulikia kesi za ukatili wa kijinsia.

**<u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>**

104. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Hivi karibuni, Meli ya Mv. Mapinduzi II imefanyiwa matengenezo makubwa sana, ili kuirejesha katika hali yake na kuwa na uwezo wa kutoa huduma bora kwa wananchi.

(a) Je, kwa sasa hali ya meli hiyo iko vipi.

(b) Ni lini meli hiyo itaanza kazi zake.

(c) Je, ni kiasi gani cha pesa kimetumika katika matengenezo ya meli hiyo hadi kukamilika kwake.

132. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Wakati wa ujenzi wa barabara ya Chake-Wete (22.1km), Mkandarasi kupitia Wizara ya Ujenzi aliwaomba wananchi na vijana wa Kisiwani, Piki na Bahanasa ndani ya jimbo la Mtambwe, wakubali viwanja vyao kuwekwa kifusi kwa makubaliano kuwa, viwanja hivyo vitawekwa sawa baada ya kukamilisha ujenzi katika eneo husika. Pamoja na moyo wa kizalendo wa vijana hawa kuruhusu jambo hili, sasa imekuwa kero na kutokujua ni lini viwanja vyao vitarudishwa katika hali nzuri ili waendelee kuvitumia kwa michezo.

(a) Je, Serikali inatambua vipi tatizo hili ambalo wananchi hawa wameshalifikisha kwa Mkandarasi mara kadhaa.

(b) Je, ni lini viwanja hivi vitatengenezwa na kurudishwa katika hali yake ya awali ili shughuli za michezo ziweze kuendelea.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

28. MHESHIMIWA AZZA JANUARI JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Wanasheria wengi wanajihusisha kikamilifu na utoaji wa mikataba ya mauziano ya viwanja pale wananchi wanapouziana maeneo yao.

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya uhalali wa Wanasheria hao kutoa mikataba ya mauziano ya viwanja.

(b) Je, kwa kiasi gani utoaji wa mikataba hiyo kunachangia kuongezeka kwa migogoro ya ardhi nchini.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

249. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Zanzibar ni nchi iliyozungukwa na bahari na shughuli kubwa za kiuchumi ni pamoja na uvuvi. Hata hivyo, mpaka sasa hakuna viwanda vya kusindika samaki tofauti na jiji kama Mwanza ambako wana viwanda viwili vya kusindika samaki ukizingatia wao wana ziwa Victoria tu.

(a) Je, kuna mpango gani Serikali itafanya wa kujenga viwanda vya kusindika samaki kwa kuwa tunao uwezo na rasilimali za kufanya hivyo.

(b) Je, Serikali imeweka mikakati gani kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuvutia uwekezaji wa viwanda vya kusindika samaki nchini.

**Wizara ya Afya:**

90. Mheshimiwa Alley Masoud Alley (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Kengeja hutoa huduma za mama waja wazito. Na kwa kuwa ni kituo pekee cha kujifungulia kinachohudumia jimbo zima na maeneo jirani. Na kwa kuwa Kituo hicho ni kidogo, hakina huduma za masaa ishirini na nne (24), hali inayoleta usumbufu kwa wanaofika kujifungua hasa kutoka shehia za Chole, Mkungu na Kengeja.

(a) Ni lini huduma ya dharura itapatikana katika Kituo hicho ili kunusuru maisha ya mama na mtoto.

(b) Kwa kuwa katika Kituo cha Afya Kengeja kuna daktari mmoja tu ambaye ni C*linical Officer*, ni hatua zipi Serikali imepanga kuzichukua katika kuongeza wataalamu wa afya kituoni hapo.

209. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha afya Jambiani ni muhimu sana kwa kutoa huduma kwa wananchi wa kijiji cha Jambiani na wageni. Hata hivyo, kituo hicho kina changamoto ya upungufu wa dawa, tatizo la jenereta, ubovu wa jiko la kuchemshia vifaa, umeme mdogo (uliopo ni *single phase*) hali inayopelekea joto katika chumba cha dawa.

(a) Je, hatua gani za haraka zitachukuliwa kutatuwa changamoto hizo.

(b) Je, ni lini Waziri na watendaji wake watakitembelea kituo hicho na kuchukuwa hatua.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

42. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu sasa, wananchi wa jimbo la Tumbe wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji safi na salama hasa kutokana na kuwepo kwa tenki moja tu linalosambaza maji katika jimbo zima. Hali inayopelekea kukosekana kwa maji katika vijiji vya Chimba, Bule, Shumba Viamboni, Kikunguni Gerei na Kinoe.

(a) Ni lini Serikali itajenga matenki mengine ya maji ya kisasa ili kuondoa tatizo la maji katika vijiji hivyo.

(b) Kwa kuwa tenki moja lililopo ni la zamani na mipira inayotumika kusambaza maji imeshazidiwa na mahitaji ya wananchi wa sasa, je, Serikali ina mpango gani wa kulifanyia marekebisho tenki hilo ili liweze kutoa huduma inayotakiwa kwa ufanisi.

(c) Ni lini Mheshimiwa Waziri utakuja kukaa na wananchi wa vijiji nilivyovitaja katika jimbo la Tumbe ili uweze kuwapa matumaini ya kutatuliwa changamoto ya maji inayowakabili.

111. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi): - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Shehia ya Sizini ni moja kati ya eneo ambalo lina changamoto

kubwa ya kukosekana maji ya uhakika kwa kuwa haina *Tank* la kuhifadhia maji.

(a) Je, ni lini hasa Serikali itawaondoshea tatizo hili wananchi wa Sizini kwa kuwajengea Tank la kuhifadhia maji

(b) Je, ni sababu zipi zinazoikwaza Serikali za kutowawekea Tank hilo, wananchi wa Sizini hadi leo hii.

(c) Je, ni gharama za kiasi gani Serikali hugharamia kwa kutumia huduma ya Direct pump ikiwa ni tofauti na gharama zinazotumika kuweka Tank.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

192. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni miongoni mwa chombo muhimu cha kutazama mwenendo na tabia za viongozi wa umma.

(a) Je, ni kesi ngapi zimeripotiwa na wananchi katika kipindi cha miaka mitano ya hivi karibuni na kesi ngapi kati ya hizo zimetolewa uamuzi.

(b) Je, kuna kiongozi yeyote aliyetiwa hatiani na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kukiuka sheria au maadili ya umma.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

18. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Je, Serikali ina mikakati ipi ya kuongeza uwakilishi wa Zanzibar katika Masoko ya Utalii hasa katika masoko ya nchi za Ulaya, Asia na Amerika, ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar kwa kila mwaka.

II. UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.

III. <u>HOJA ZA SERIKALI</u>

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:</u>**

Mjadala wa Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la Kumi na Moja la Wawakilishi iliyotolewa tarehe 10 Novemba, 2025 na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Zanzibar,
12 Februari, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
<u>WAWAKILISHI, ZANZIBAR</u>